# JINSI YA KUWA



# ...MTOTO WA Mungu





Toleo la Kushuhudia

Linajumuisha: *Jinsi ya Kutoa Ushuhuda Wako na Jinsi ya Kushuhudia*

# Jinsi ya Kuwa Mtoto wa Mungu

## David Howell

### Toa Msaada kwa Huduma Hii

Prison Evangelism huchapisha na kusambaza kitabu cha Jinsi ya kuwa Mtoto wa Mungu bila malipo kwa magereza 2100 nchini Marekani yenye idadi ya wafungwa 2,000,000. Kusudi letu ni kubadilisha mioyo ya watu na kufunga magereza. Kusudi hilo linatimizwa kwa kumwamini na kumpenda Yesu Kristo. Bila badiliko la mioyo asilimia sabini ya wafungwa watarudi gerezani ndani ya miaka mitano.

Tusaidie kuweka wafungwa huru kikamilifu kwa kutoa msaada wako wa kifedha.

Unaweza kununua vitabu kwa ajili ya huduma yako mwenyewe kupitia:
**howtobeachildofgod.com**
Faida zote za kifedha zitatumiwa kununulia magereza vitabu zaidi.

Unaweza kutoa mchango wako kwa huduma hii moja kwa moja kupitia:
**prisonevangelism.com**

Facebook: @ Prison Evangelism, Inc. na @How to be a child of God

Pia unaweza kutuma cheki kwa: Prison Evangelism
PO Box 571977
Houston, Texas 77257

Hakimiliki © 2019 ya David Howell

Haki zote zimehifadhiwa. Hakuna sehemu ya chapisho hili inaweza kutolewa upya kwa namna yoyote ile bila idhini ya maandishi kutoka kwa David Howell

Kitabu hiki kinaweza kununuliwa kwa wingi kwa ajili ya madhumuni ya kielimu na kiinjilisti. Tafadhali wasiliana na mchapishaji kwa taarifa zaidi.

David Howell
PO Box 571977
Houston, Texas 77257 davidhowell@aol.com
info@HowtobeaChildofGod.com www.
HowtobeaChildofGod.com

SOMA KITABU HIKI CHA KIELEKTRONIKI (EBOOK) NA UTAZAME VIDEO HII KATIKA @ WWW.PRISONEVANGELISM.COM

Isipokuwa iwe imetajwa, nukuu zote za Maandiko ya Biblia zimetolewa kutoka katika Biblia ya Swahili Union Revised Version ya 2005, iliyochapishwa na Chama cha Biblia cha Kenya na Chama cha Biblia cha Tanzania.

ISBN: 978-0-578-14157-2

Mwelekezo wa usanifu umetekelezwa na John Magee, Houston, Texas, JohnMageeDesign.com

Michoro yote imechorwa na Randy Rogers, The Woddlands, Texas, artistguy@att.net

# UTANGULIZI


"Kwa kweli, tukipewa mafunzo kamili kuhusu Kristo na Msalaba wake hapo mwanzoni, tunaweza kushuhudia matukio makuu kuanzia siku ya kwanza ya maisha yetu ya Kikristo, ingawa maelezo kamili ya matukio hayo yatafuatia baadaye."

Watchman Nee, The Normal Christian Life

Tunapomwamini Yesu Kristo kama Bwana, Mungu, Mwokozi na Uzima, pia tunamuomba atawale nia zetu na maisha yetu. Hakika anakuwa uzima wetu. Tunabadilishwa; wakati mwingine haraka, wakati mwingine polepole, lakini mabadiliko lazima yatatokea. Roho wa Mungu mwenyewe anakuja kuishi ndani yetu na anatufanya tuwe wazima, wenye uhai na kamili. Maisha hayawezi kubakia jinsi yalivyokuwa tunapoamini na kutoa mioyo yetu kwa Mungu.

David Howell

Mungu alikuwa Mbinguni na alikuja duniani kama mwanadamu.



Wafilipi 2:6-8, Yohana 1:14, Waebrania 1:3, Warumi 8:3b, Yohana 10:30, Wakolosai 1:15, Wakolosai 2:9, Waebrania 2:11-17, Mathayo 1:20-21


Mimba yake ilitungwa kimuujiza, lakini alizaliwa na mwanamke sawa na sisi.
Alifanya hivyo ili tuweze kuwa na uhusiano wa kibinafsi na yeye na kumjua kama Mungu na mwanadamu na kumwelewa vyema kama Baba.

Yesu alipitia utoto na ujana, akajifunza ujuzi maalum, na wakati wake ulipofika, alianza huduma ambayo alikuwa amekuja kutekeleza, ambayo ni kujifunua kwetu sisi sote kama Mungu na Mwokozi



Mathayo 3:13-17, Mathayo 7:28-29, Marko 6:2-3, Luka 2:40, Luka 2:41-47, Luka 2:52

Kusudi lake duniani lilipokamilika, kwa hiari yake alikubali kusulubiwa.



Alidhalilishwa na kuteswa kisha akatundikwa msalabani kwa misumari. Yesu alichagua kufa kifo hicho cha kikatili zaidi ili mimi na wewe tusilazimike kulipia adhabu ya makosa yetu. Alitaka tujitambulishe na yeye na yale aliyoyapitia. Kwa njia zinazojulikana na Mungu pekee, damu ya Yesu Kristo na kujitoa kwake



kama dhabihu kunaweza kuosha dhambi zetu na kututakasa milele. Kitendo hicho cha upendo mkamilifu kilitufanya tuwe watakatifu ili Mungu atuone sisi kama watoto wake kama vile anavyomwona Yesu.


Mathayo 26:28-29, Mathayo 27:57- 61, Warumi 5: 6, Warumi 8:3, Waefeso 1:7, Waebrania 2:14 -15, Waebrania 9:22, 1 Petro 2:24, 1 Yohana 1:7




Yesu alikuja ili tuweze kuanzisha uhusiano wa kibinafsi na yeye na atupatie karama yake ya uzima wa milele. Uzima wa milele ni uzima wa Kristo. **Hauna mwanzo wala mwisho.**

Luka 24:1-7, Luka 24:50-51, Yohana 16:28, Waebrania 1:3

Kwa nini hayo yote yalikuwa muhimu? Kwa sababu Mungu alipoumba mtu wa kwanza, Adamu, alimpa maisha mazuri sana Paradiso lakini Adamu hakumtii Baba yake wa Mbinguni.




Kuanzia hapo, mwanadamu alikuwa na mwili na nafsi (utu), lakini kwa Mungu alikuwa amekufa kiroho. Hakuwa mzima na hakuweza tena kupata baraka ambazo Mungu alikuwa amemuandalia.

Mwanzo 2:8-9, Mwanzo 3:2-6, Mwanzo 2:16-17, Mwanzo 3:23, I Wakorintho 15: 45-46

Sisi kama watoto wa wazazi wetu ambao kizazi chao kinarudi nyuma hadi kwa Adamu, tulikufa kiroho pamoja na Adamu katika bustani ya Edeni.



Tumebeba mizigo ya kizazi hicho pamoja na mizigo ya dhambi zetu wenyewe na mizigo ya kihisia ambayo inaingia maishani mwetu kadiri tunavyoendelea kuishi duniani. Ni mizigo ya vitu kama aibu, kujiona mwenye hatia, matatizo ya zamani na hisia mbaya juu ya dhambi zetu na kasoro za kitabia. Tunahitaji kizazi kipya na familia mpya.


Warumi 3:23, Warumi 5:12, Warumi 5:18a



Siku moja, mtu fulani alikuja na akaeleza simulizi ya maisha ya Yesu, jinsi alivyokuja kutuokoa kila mmoja wetu kutokana na mauti ya milele kwa kutufia na kutupatia uzima wake wa milele. Yesu alikufa na akatupatia sisi sote suluhu, ambayo ni njia ya kupata msamaha kikamilifu, upendo usio na masharti, na tumaini la uzima wa milele kupitia yeye.

Ezekieli 36:26-27, Matendo 4:12, Warumi 5:9, 1 Wakorintho 15:57, 2 Wakorintho 5:18a, Wagalatia 1:15-16, Waefeso 2:8-9, 1 Timotheo 2:5-6

Yesu pia alikuja ili mimi na wewe tuweze kuwa na amani na uzima tele hapa duniani kwa njia ya uhusiano na yeye. Anataka kutuonyesha jinsi ya kukabiliana na matatizo ya maisha. Yesu anatoa tumaini na namna mpya wa kuishi. Njia zetu kama wanadamu hutuweka katika hali ya ubinafsi na msukosuko. Hazijawahi kutusaidia.



Yohana 10:10, Warumi 6:16, Warumi 6:21, Warumi 8:37, Waefeso 2:14, Ufunuo 3:20



Hatuwezi kuwa na amani wakati tumetenganishwa na Mungu. Maamuzi tunayofanya kila siku ni yenye ubinafsi na yanatuweka katika hali ya kufadhaika na kutenganishwa na ushirika na Mungu. Tuna hamu kubwa ya kuunganishwa na Baba yetu wa Mbinguni katika uhusiano wenye amani, lakini hatuna uhusiano wa kiroho naye. "Fikira zetu bora zaidi" na nia zetu nzuri ndizo zilizotuingiza katika mashaka haya.

Mhubiri 3:11, Warumi 6:16, Luka 1:78-79, Yohana 16:33, Warumi 5:1-2, Warumi 8:6

Tunajaribu kupata suluhu ya pengo linalotutenganisha na Mungu na tunatafuta njia za kurudisha tena uhusiano naye. Njia hizo hazitusaidii. Ni kwa kumwamini Yesu Kristo pekee ndipo tunaweza kuwasiliana na Mungu Baba.





Mithali 14:12, Warumi 6:23, Warumi 3:23



Huyu ni Yesu yule yule ambaye alikufa kwa ajili ya dhambi zetu, makosa yetu, na kasoro zetu zote za kitabia; za zamani, za sasa na za baadaye. Kupitia damu yake, tunaweza kusafishwa na kufanywa kuwa sawa mbele za Mungu. Tunaweza kupokea msamaha kikamilifu na upendo usio na masharti kutoka kwa Mungu Baba. Kupitia kifo chake na kufufuka kwake, Yesu aliondoa pengo kati ya Mungu na mwanadamu. Ndio maana yeye ndiye Mwokozi wa Ulimwengu.

Yohana 3:16, 1 Petro 3:18, 1 Timotheo 2:5-6, Warumi 5:1

Sote tunayo nafasi ya kukubali au kukataa ukweli huo. Ikiwa tutakubali kwamba matukio hayo ni ya kweli na tunamwamini Yesu kama Mungu, tunakuwa watoto wa Mungu, na tunapewa haki na faida zote alizo nazo Yesu. Tunakuwa warithi wenza pamoja naye na pia tunakuwa kaka au dada wa Yesu Kristo. Weka nia zako na maisha yako mkononi mwa Yesu bila kuwa na wasiwasi wowote. Si jambo gumu, lakini hatua hiyo huenda ikawa mojawapo ya mambo magumu zaidi ambayo umewahi kufanya. Ikiwa kweli unataka kupata ahadi za Mungu na furaha inayotokana na kuwa na ushirika pamoja naye, muombe atawale maisha yako. Ukiomba kwa uaminifu, sala rahisi zaidi itatosha... kwa sababu Mungu huzingatia mioyo yetu. Toa maisha yako kwake kupitia sala hii rahisi. HIYO PEKEE NDIO INAYOHITAJIKA UNAPOMTUMAINIA MUNGU NA KUMUAMINI!






Waefeso 2:13, Yohana 14:6, Waebrania 4:3, Waebrania 4:7

"Baba wa Mbinguni, najitoa kwako---
-unibadilishe na ufanye kile unachotaka na mimi. Chukua udhibiti wa maisha yangu na uniondolee njia zangu za ubinafsi, ili nifanye mapenzi yako. Nipe ushindi dhidi ya dhambi yangu ili niwe mfano kwa wale nitakaowasaidia kupitia Nguvu yako na Upendo wako. Ninajisalimisha katika Namna yako ya Maisha. Naomba nikuamini na nifanye mapenzi yako wakati wote! Njoo Bwana Yesu na uishi maisha yako kupitia mimi. Amina."



Sema kwa kinywa chako na uamini moyoni mwako kwamba Yesu alikufa, akazikwa, na akafufuka kutoka kwa wafu. Mwamini kwamba yeye ni Mungu katika mwili na uwe Mtoto wa Mungu na mrithi mwenza pamoja na Kristo.

Yohana 11:25-26, Yohana 14:6-7, Warumi 10:9, Warumi 10:13, 1 Wakorintho 6:17, Waefeso 1:5-8, Waefeso 2:8-10, Wakolosai 2:6-7, 1 Yohana 5:12-13


Kadiri unavyopokea Roho wa Mungu, unakuwa mzima na hai kwa Mungu.

Unapomwomba Yesu Kristo aingie maishani mwako, unahamishwa kutoka kwenye kizazi cha familia yako ya kidunia ya Adamu na unaingizwa kwenye uzima wa milele wa Kristo, **ambao ni uzima usio na mwanzo wala mwisho.** Unawekwa msalabani na utu wako wa zamani unakufa pamoja na Kristo.



Warumi 5:18-19, Warumi 8:1-2, 1 Wakorintho 15:22, Wagalatia 5:24, Waefeso 1:13-14, Waefeso 3:14-15, 1 Petro 1:18-19



Unakuwa kitu kimoja na yeye. Unaunganishwa na Kristo na hali hiyo haitabadilika kamwe. Yesu sasa anaishi ndani yako na wewe ndani yake. Popote aendapo, nawe unaenda. Popote uendapo, naye anaenda.

Yohana 14:20, Warumi 6:6, Wagalatia 2:20, Wagalatia 4:4-7, Wagalatia 5:24, Waefeso 1:11, Wakolosai 2:10

Wakati «utu wako wa zamani» ulikufa pamoja na Yesu Msalabani, pia ulizikwa pamoja naye. Utu wako mpya wa kiroho unapata kuwa hai pamoja na Kristo na unaenda pamoja naye Mbinguni. Uliacha nyuma mizigo yako ya kasoro, kujiona mwenye hatia, dhambi na aibu. Uko ndani ya Kristo naye yuko ndani yako. Unabadilisha maisha yako ya zamani na maisha mapya. Sasa Roho wa Mungu yuko ndani yako na roho yako ya kibinadamu imerejeshwa katika uhai pamoja na Mungu. Uko ndani ya Kristo na umeanza safari nzuri ya uzima wako wa milele. UMEZALIWA UPYA!



Yohana 3:6, Yohana 11:25-26, Warumi 5:5, Warumi 6:4-6, Warumi 8:10, Wakolosai 2:12-14, Wakolosai 3:1-3, Waefeso 1:13b, Waefeso 2:6



Kama ulikuwa mwaminifu katika sala yako, sasa wewe ni sehemu ya familia mpya --- Familia ya Mungu. Mungu Baba anatukubali sisi sote kama watoto wake na tunakuwa warithi wenza pamoja na kaka yetu mkubwa Yesu. Anakukubali na anakupenda bila masharti yoyote kama sehemu ya familia yake. WEWE NI MTOTO WA MUNGU!

Zaburi 16:11, Warumi 5:11, Warumi 8:15-17a, 2 Wakorintho 5:17, Wafilipi 3:20a, Waebrania 2:11-12, Ufunuo 21:2

Utu wako wa zamani ulikufa msalabani pamoja na mizigo ya dhambi iliyobebwa na Kristo. Unaweza kufurahi kwamba huhitaji tena kufungwa na dhambi, uraibu, na njia zingine za ubinafsi za mwanadamu. Ulikufa pamoja na Kristo na huwezi kutishiwa tena na mauti kwa sababu silaha ya Shetani ya hofu haina nguvu tena.



Ujasiri mpya unaingia maishani mwako baada ya kupata uzima wa milele. Mauti haina ushawishi wala haiwezi tena kutawala maisha yako. Kristo alikufa kwa ajili ya dhambi zetu za kusema uongo, kuiba na mambo mengi mengine. Tulikufa pamoja naye ili kujitenga na asili yetu ya dhambi. Tuna uhuru wa kuchagua kufanya vitu kwa njia zetu au kwa njia ya Mungu. Hatukuwa na chaguo hilo kabla ya kuweka nia zetu na maisha yetu mkononi mwa Mungu kupitia Yesu Kristo.

Warumi 6:11-13, Warumi 8:1-2, Warumi 8:15-17a, Wagalatia 5:16, Wakolosai 2:6-7, 2 Timotheo 1:7, Waebrania 2:14-15



Inaweza kuwa vigumu kwetu kuelewa kikamilifu ukweli huo kwani miili yetu na nafsi zetu---yaani utu wetu---bado zinaishi maisha haya ya hapa duniani. Lakini sasa Roho wa Kristo anaishi ndani yetu na sisi ni viumbe wa kiroho. Ikiwa tutakuwa na uzima tele ambao Mungu anataka tuwe nao, basi lazima tukubali mambo hayo kwa imani. Badilisha mawazo yako na uweze kuona wewe ni nani na uko wapi. Weka fikira zako katika mambo ya Mbinguni ya Baba yako na si katika takataka za maisha yetu ya kila siku hapa duniani. Utapata furaha kamili kuwa katika Familia ya Mungu. Utu wako wa zamani ulikufa na una maisha mapya katika Yesu Kristo. Ni njia mpya kabisa ya kufikiria. UNABADILISHWA!

Warumi 8:5-6, Warumi 12:2, 1 Wakorintho 2:16, Waefeso 2:6, Wafilipi 2:5, Wafilipi 3:20a, Wafilipi 4:6-8, Wakolosai 3:1-3, 2 Timotheo 1:7

Urithi wetu uko katika kizazi cha wazazi wetu wa kibaiolojia na Adamu au uko katika Familia ya Mungu. Hakuna chaguo zingine kando na hizo mbili. Bila imani katika Yesu Kristo, kila mmoja wetu anasalia katika Adamu.



Waumini wengi hufikiria wanaweza kuweka mguu mmoja katika kizazi cha Adamu (au ulimwengu wa familia yetu ya kidunia) na mguu mwingine katika Familia ya Mungu. Matokeo yake ni mgogoro ndani ya nafsi na msukosuko wa kiroho. Kukosa kufanya uamuzi thabiti hutuacha tukiwa tumechanganyikiwa bila kupata ushindi ambao Mungu ametupangia.

Mathayo 7:13-14, Warumi 6:16, Warumi 7:14-25, Warumi 8:1-2, 1 Wakorintho 15:22, Wagalatia 5:16, Wafilipi 3:20

Kama vile Mungu alivyo katika nafsi tatu, (Baba, Mwana na Roho Mtakatifu) sisi pia tuko katika sehemu tatu . Tunaishi katika miili inayohusiana na mazingira yetu kupitia hisia zetu za kimwili. Tuna nafsi ambayo ni utu wetu na imebeba akili, nia na hisia zetu. Na sisi ni roho ambayo sasa imefanywa kuwa hai kupitia imani yetu na ufahamu wetu wa Yesu uliowezeshwa na kifo chake msalabani, kuzikwa kwake na ufufuko pamoja naye. Roho ndio sehemu yetu ambayo ina uhusiano na Mungu.



Mwanzo 2:7, Mathayo 3:13-17, Yohana 3:6, Warumi 8:10, 1 Wakorintho 3:16 -18, 1 Wathesalonike 5:23 -24, Waebrania 4:12

Jukumu letu ni kujisalimisha kikamilifu kwa Yesu Kristo. Anachotaka ni kuishi maisha yake ndani yetu na kupitia sisi ili kutimiza kusudi lake hapa duniani.



Sisi kwa kweli ni Mwili wa Kristo na anataka kutumia kila mmoja wetu kufikia wengine na kupanua Familia. Karibu katika Familia ya Mungu. Wewe ni kiumbe kipya! Sema "kwaheri" kwa utu wako wa zamani na, "jambo" kwa utu wako mpya, ambaye ni Yesu Kristo anayeishi ndani yako.

Warumi 6:11-13, Warumi 8:10, Warumi 12:1, Warumi 12:4-5, 1 Wakorintho 3:16, 1 Wakorintho 6:19-20, 2 Wakorintho 5:16-21, Waefeso 4:21-24, Wafilipi 2:5-8, Wakolosai 1:27, 1 Yohana 3:1-3, 1 Yohana 3:9-10, 1 Yohana 5:18-19

Kama mtoto wa Mungu na mrithi mwenza pamoja na Yesu, unaanza kushiriki urithi pamoja naye na unapata kionjo cha kuwa na uzima tele. Unapokuwa na roho mpya wa Mungu ndani yako, utataka kujifunza mengi zaidi juu ya njia za Mungu ili uweze kumfuata. Mungu amejifunua kikamilifu katika Mwanawe, Yesu. Kwa hivyo jifunze yote unayoweza juu ya Yesu. Chukua Biblia na usome Agano Jipya juu ya maisha ya Yesu. Kitabu cha Yohana ni mahali pazuri pa kuanzia. Sura kumi na mbili za kwanza za kitabu cha Mwanzo katika Agano la Kale zinaelezea jinsi mambo yote yalivyoanza. Angalia kumbukumbu zilizo chini ya kurasa za kitabu hiki ukitumia Biblia yako binafsi au angalia vifungu vya Biblia katika sehemu ya kumbukumbu ya kitabu hiki ili uelewe vyema kile kinachosemwa kwenye kila ukurasa.



- Ongea na Baba yako mpya kila siku katika sala. Mshukuru kwa maisha yako mapya na familia yako mpya. Ongea naye kwa uwazi na kwa undani kama rafiki, kana kwamba amekaa kando yako. Mfikirie katika mfano wa Yesu, ambaye unaweza kuhusiana naye kama kaka yako mkubwa.
- Soma Biblia. Kwa kuwa sasa una roho mpya, yaani Roho wa Mungu ndani yako, utapokea uelewa mpya wa kile ambacho maandiko yanamaanisha. Maandiko ya Biblia ni Neno la Mungu na ni jinsi Baba yako mpya anavyonena nawe. Anakupenda zaidi ya jinsi unavyoweza kufikiria.
- Tafuta kanisa, kundi la washirika wa Kikristo na/au mkutano wa mafundisho ya Biblia ambapo unaweza kukutana na wengine na uendelee kujituma mahali hapo kadiri unavyozidi kukua katika imani yako. Mara nyingi Baba yako wa Mbinguni atanena nawe kupitia waumini wengine.
- Ubatizo wa maji unapaswa kufuata mara tu baada ya kujitolea kwako kwa Yesu. Ubatizo ni kitendo cha kuiga, kutii, na kujitambulisha na Yesu.
- Pata mfadhili Mkristo, mtu atakayekufunza kuwa mwanafunzi wa Yesu au mshauri ambaye unaweza kujifunza kutoka kwake na kuwajibika kwake.
- Nenda uwaambie wengine juu ya imani yako mpya katika Yesu.
- Tunapendekeza ununue Biblia. Hasa, Biblia ya Swahili Union Revised Version (SURV) iliyochapishwa na Chama cha Biblia cha Kenya na Chama cha Biblia cha Tanzania.

Mungu aibariki safari yako ya kiroho!


Yoshua 1:8, Mathayo 3:13-17, Mathayo 7:7-8, Mathayo 10:32, Yohana 14:13-14, Yohana 15:7, Wafilipi 4:6-7, Waebrania 4:12, Yakobo 5:15-16, 1 Yohana 1:9

Wala msifuate kanuni za dunia hii; bali mgeuzwe kwa kufanywa upya nia zenu, mpate kujua hakika mapenzi ya Mungu yaliyo mema, ya kumpendeza, na ukamilifu.
Warumi 12:2



Na kwa sababu mimi ni hai, nyinyi nanyi mtakuwa hai. Siku ile ninyi mtatambua ya kuwa mimi ni ndani ya Baba yangu, nanyi ndani yangu, nami ndani yenu.

Yohana 14:19b-20




Tulisulubiwa pamoja naye, tukazikwa pamoja naye, tukafufuliwa pamoja naye na sasa tumeketi pamoja naye katika uwepo wa Mungu mwenyewe.



Akatufufua pamoja naye, akatuketisha pamoja naye katika ulimwengu wa roho, katika Kristo Yesu,

Waefeso 2:6



Nimesulubiwa pamoja na Kristo; lakini ni hai; wala si mimi tena, bali Kristo yu hai ndani yangu; na uhai nilio nao sasa katika mwili, ninao katika imani ya Mwana wa Mungu, ambaye alinipenda, akajitoa nafsi yake kwa ajili yangu.

Wagalatia 2:20

# Kwa vile sasa wewe ni Mtoto wa Mungu . . .

Wewe kama mtoto mpya wa Mungu, una faida zote za kuwa mwana au binti yake. Unaweza kuwa na ushirika na Mungu, umwite Baba, ukae miguuni pake, umfungulie moyo wako na kwa jumla umruhusu awe Baba yako akupendaye daima, rafiki yako, mtoshelezaji wa mahitaji yako, na mwandani wako. Pamoja na faida hizo kuna majukumu pia na baadhi ya majukumu hayo yataelezwa katika kurasa chache zinazofuata. Unaagizwa uende na umwambie mtu mara tu baada ya kumpokea Kristo.

**Basi, kila mtu atakayenikiri mbele ya watu, nami nitamkiri mbele za Baba yangu aliye mbinguni. Mathayo 10:32**

Tatizo ni kwamba, hatujafundishwa jinsi ya kufanya hivyo, lakini ni mchakato rahisi na umeelezwa katika kurasa chache zinazofuata za **Jinsi ya Kutoa Ushuhuda Wako**. Cha muhimu ni kuwa tayari kufanya hivyo na ni jambo rahisi kufanya ikiwa ulikuwa mwaminifu ulipomwomba Yesu achukue udhibiti wa nia zako na maisha yako. Yesu yuko ndani yako wakati huu akifanya mabadiliko katika jinsi unavyofikiria, jinsi unavyofanya maamuzi na jinsi unavyohisi. Kutoa ushuhuda wako ni rahisi kama vile kusema **Nilikuwa kipofu na sasa naona (Yohana 9:25)**. Unapotoa ushuhuda wako, unakuwa mtiifu na unafanya kile ambacho Mungu anataka ufanye. Unaanza maisha yako mapya. Kumbuka, si wewe uliye hai, bali ni Kristo aliye hai ndani yako, kwa hivyo uwe tayari kumruhusu anene kupitia wewe.



# . . . Waambie wengine!

Pia tumepewa jukumu la kuwafanya wengine wamjue Yesu Kristo na kupanua ufalme wa Mungu. **(Kwa kuwa Mwana wa Adamu alikuja kutafuta na kuokoa kile kilichopotea. Luka 19:10.)** Wewe ni sehemu ya mwili wa Kristo na unaweza kutekeleza jukumu hilo kupitia maagizo yaliyo kwenye kurasa chache zinazofuata. Cha muhimu ni kuwa tayari kufanya hivyo. Lazima uwe tayari kutekeleza jukumu hilo ili Yesu Kristo aishi maisha yake kupitia wewe na awafikie wengine. Labda Yesu hakuambii uende kuzungumza na watu usio wafahamu, bali uwafikie watu ambao tayari unawafahamu, ambao umekuwa ukiwaona na umekuwa ukiwatembelea mara kwa mara. Yesu tayari ameshawachagua na unapofikiria juu ya mtu ambaye unafikiria angependa kumfahamu Yesu, unaanza kufikiria kama Kristo. Sehemu ya **Jinsi ya Kushuhudia** inakufundisha jinsi ya kumwongoza mtu kumjua Yesu Kristo na kuwa na amani na Mungu. Maagizo ya kufanya hivyo si magumu. Kile kinachohitajika ni utayari wako na hamu yako ya kumruhusu Yesu Kristo kuishi maisha yake kupitia wewe.



**Basi, kabla ya mambo yote, nataka dua, na sala, na maombezi, na shukrani, zifanyike kwa ajili ya watu wote. 1 Timotheo 2:1**




Najua neno moja, kuwa mimi nilikuwa kipofu na sasa naona.
Yohana 9:25

# Jinsi ya Kutoa Ushuhuda Wako

## Ushahidi wa Kikristo kupitia Ushuhuda wa Binafsi

Kushiriki ushuhuda wako binafsi wa jinsi ulivyokuja kumjua na kumwamini Yesu Kristo ni hatua ya kwanza ya kutekeleza uinjilisti wa kibinafsi. Kuna aina mbili za ushuhuda wa kibinafsi. Moja ni ushuhuda wa kihistoria, ambao unaeleza juu ya maisha yako kabla, wakati na baada ya kumjua na kumwamini Yesu Kristo kama Bwana na Mungu, na Mwokozi wa roho yako. Ushuhuda mwingine ni ule unaozingatia mada fulani na unaweza kuwa tukio la wokovu wako na jinsi ambavyo maisha yamekuwa tangu wakati huo. Ushuhuda huu unaweza kutolewa na mtu ambaye alimpokea Kristo akiwa mtoto na anaweza kutoa taarifa kuhusu maisha yake tangu alipookoka. Mfano mwingine unaweza kuwa mtu ambaye alikuwa ameamini kuwa yeye ni Mkristo maisha yake yote lakini akagundua kuwa hakumjua Mungu kisha akachukua hatua ya kujisalimisha kwa Mungu na kutubu.

*ANZA USHUHUDA WAKO KWA KUTAJA JAMBO FULANI LINALOKUUNGANISHA NA MSIKILIZAJI WAKO; PENGINE MNATOKA MJI MMOJA, MNAFANYA KAZI MOJA, MLIENDA SHULE MOJA NA KADHALIKA. TAFUTA VITU AMBAVYO WEWE NA MSIKILIZAJI WAKO MNAVIPENDA.*

# Jinsi Maisha Yako Yalivyokuwa

Unapotoa ushuhuda wako, unasimulia na kuelezea kwa ufupi juu ya matukio yaliyokufanya utake kubadilisha jinsi unavyofikiria na kuendesha maisha yako. Sote tumefanya maamuzi mabaya maishani ambayo tunatamani hatungefanya na tungependa kufanya mambo fulani upya. Tunatamani tungepata nafasi ya kuishi maisha yetu upya. Wakati mwingine, ni mfululizo wa matukio fulani ndio uliotufanya tutafakari juu ya maisha yetu au inaweza kuwa ni kosa moja kubwa au tukio lisilotarajiwa ndilo lilitufanya tutafakari juu ya maisha yetu. Haijalishi ni hali gani, matokeo ya matendo yetu au tabia zetu yanaweza kuwa ndio kichocheo kinachotufikisha mahali ambapo hatuwezi kutegemea nguvu zetu binafsi. Ni wakati unapojua kwamba huwezi kuendelea kuishi kwa njia ile ile na ni sharti ufanye mabadiliko la sivyo utalipa gharama kubwa. Huenda tayari umeshafikia mahali ambapo unalipia gharama ya maamuzi yako. Wengi wetu hufikia mahali katika safari zetu za maisha ambapo tunajua kwamba hatuwezi tena kutegemea nguvu zetu binafsi. Nguvu zetu binafsi hazitusaidii. Tunahitaji kujua Mungu wa kweli ni nani kisha tuache kujaribu kutekeleza majukumu ya Mungu katika maisha yetu.



# Kile Kilichotokea

Wakati tumejinyenyekeza na tukagundua kwamba sisi si wadhibiti wa ulimwengu, tunaanza kutafakari juu ya maamuzi tunayoweza kufanya. Kwa njia ya kushangaza na ya kimuujiza, mtangazaji wa injili atajitokeza, mtu atakayekuambia juu ya maisha bora ya milele na jinsi ya kuwa na amani na Mungu. Anaweza kuja kama rafiki au jamaa au mtoto, kaka au dada. Anaweza kukuomba uambatane naye kanisani au katika mkutano wa mafundisho



ya Biblia. Anaweza kukushuhudia (kupitia ushuhuda wake binafsi) na kupendekeza ujaribu njia ya kiroho zaidi katika kukabiliana na shida zako, kama kumtafuta Yesu kwanza na kukiri kwamba huwezi kuendelea na maisha yako kwa nguvu zako binafsi. Lakini kuna kitu



kitakachokuvutia unapomtafuta Mungu na unapokuwa tayari hatimaye kujisalimisha na kukubali njia mpya ya maisha. Unataka kuwa mtoto wa Mungu kwa njia zote zinazowezekana. Hali hiyo inatokea maishani mwako. Umefanya uamuzi wa kumwamini Bwana Yesu Kristo na umemwomba atawale nia zako na maisha yako. Maisha mapya yameanza.

# Jinsi Maisha Yako Yalivyo Sasa


Umekuwa mtoto wa Mungu, muumini aliyezaliwa upya. Unampenda na kumwamini Bwana Yesu Kristo kama Bwana, Mungu, Mwokozi na Uzima. Maisha yako yamebadilika na uko kwenye njia sahihi ukiwa na mtazamo mpya na maadili mapya. Sasa unawajibika kwa Baba yako wa mbinguni. Katika sehemu hii unasimulia jinsi maisha yako yamebadilika na jinsi mawazo yako na hata utu wako umebadilika. Eleza jinsi neema ya Mungu inavyokuandaa kukabiliana na shida za maisha na jinsi Roho wa Mungu anavyokuongoza kufanya kile kilicho sahihi na anavyokurekebisha unapopotoka. Unaweza kuelezea mazuri na mbaya katika sehemu hii. Tunajua mambo hayawi mazuri wakati wote. Jambo la muhimu ni kwamba Kristo ndani yako anafanya kazi na wewe ni kazi inayoendelea.



# Ni nini Kitakachofuata







Tunakua katika Kristo kuanzia hapa na kuendelea mbele. Wakati mwingine safari imejaa milima na mabonde, lakini tunavyo vifaa vipya vya kukabiliana na vizuizi na shida tunazokutana nazo. Tuna nguvu ya Mungu kupitia Roho Mtakatifu aliye ndani yetu kutuonyesha njia na kutuepusha na kufanya maamuzi mbaya ya maisha ya zamani. Tunasoma Biblia na tunajifunza kumuiga Kristo kwa kujifunza njia zake na tabia zake. Tunakuja kugundua na kuelewa kwamba wakati Kristo alikufa, utu wetu wa zamani ulikufa pamoja naye na sasa sisi ni viumbe wapya. Tunahitaji tu kujua na kuelewa kuwa Yesu Kristo anaishi ndani yetu na tutumie ukweli huo wa msingi kadiri tunavyoendelea kuokolewa na kubadilishwa kuwa katika mfano wake. Unaanza kumuiga Mwokozi aliyefufuka kadiri unavyozidi kukomaa kama Mkristo. Unaanza kugundua kuwa Yesu Kristo, ambaye ni Mungu aliyefufuka, anatafuta kuishi maisha yake ndani yako na kupitia wewe ili kutimiza matakwa yake pamoja na wale ambao ni wake, yaani watoto wa Mungu. **Unazidi kuwa kama Kristo, unaacha nyuma maisha ya zamani na kumfuata.**




Zaburi 40:3, Yohana 9:25, Yohana 12:17, Wakolosai 4:5-6, 1 Wathesalonike 1:6-8, 1 Petro 3:15, Ufunuo 12:11, Ufunuo 19:10



# Jinsi ya Kushuhudia

**Maagizo ya kumtambulisha Yesu Kristo kwa mtu asiyeamini.** Mapendekezo kumi yafuatayo ni njia yenye ufanisi ya kuwasilisha ujumbe wa msalaba. Fuata maagizo kwa uangalifu na utafaulu. Utaweza kuwa bora katika kupanda mbegu na kuleta nafsi za watu kwa Mungu. Katika hali zote, utashiriki katika kupanua ufalme wa Mungu na hilo ndilo kusudi la msingi la maisha yako.

• **Fikiria watu kumi.** Watu hao huenda ni marafiki, jamaa, wapendwa au watu unaohusiana nao katika biashara au katika maisha ya kila siku mahali unaponunua bidhaa, mahali unapocheza na mahali unapofanya kazi.

• **Andika majina yao.** Ukishamaliza kuandika majina kumi maalum kwenye karatasi, bandika karatasi hiyo mahali ambapo utaweza kuona majina hayo kila siku.

• **Anza kuomba kwa ajili ya wokovu wa kila mmoja wa watu hao.** Unapoomba, mwombe Mungu afungue akili na mioyo yao ili wasikie juu ya Yesu na uzima wa milele. Kumbuka, lengo letu si kuwafanya watu wabaya wawe wazuri, bali kuwafanya watu waliokufa kiroho wawe hai kwa kuwapa zawadi ya uzima wa milele ambao umepokea.

• **Endelea kuombea kila mmoja wao kwa siku ishirini na moja.** Mungu hajali kipimo cha wakati unaotumia kuombea roho hizi maalum, lakini tunajua inachukua siku ishirini na moja kuanzisha tabia. Kwa hivyo, hakikisha umewaombea watu hao kwa kipindi hicho cha muda. Basi utakuwa umeanzisha tabia yenye nguvu ya kuwaombea waliopotea.



• **Anza kuwasiliana na kila mmoja wao.** Baada ya siku ishirini na moja, utakuwa umefunika watu hao kwa maombi na sasa ni wakati wa kuchukua hatua. Mpigie simu mtu wa kwanza na umwambie una kitu cha kumuonyesha na unataka kuona kama kina maana kwake. Mualike rafiki yako kwa kahawa au chakula cha mchana. Endelea kumpigia simu au kuwasiliana naye mpaka aseme <Ndiyo>.

• **Onyesha kitabu cha Jinsi ya kuwa Mtoto wa Mungu.** Mwambie rafiki yako kwamba uliona kijitabu fulani na kimekugusa na ungependa kuona kama kinaweza kuwa na maana yoyote kwake. Ikiwa una kompyuta au iPad au kifaa kingine cha mkononi, unaweza kwenda katika: www.howtobeachildofgod.com na usome kitabu hicho cha kielektroniki (yaani ebook) au utazame uwasilishaji wa video ikiwa huna nakala ya kitabu chenyewe.

• **Pitia kitabu chote ukurasa kwa ukurasa.** Soma sala iliyo kwenye ukurasa wa 14, lakini endelea hadi mwisho wa kitabu. Onyesha rafiki yako maandiko yaliyo nyuma ya kitabu, ukielezea kwamba yamewekwa hapo ili aweze kuyasoma kwa urahisi ikiwa hana Biblia. Onyesha jinsi maandiko hayo yanavyoeleza au yanavyothibitisha maandishi au mifano iliyo katika kitabu.

• **Toa ushuhuda wako.** Katika hatua hii, anza kusimulia kisa chako au ushuhuda wako wa jinsi ulivyokuja kumjua Yesu Kristo. Ushuhuda unaelezea: *JINSI MAISHA YAKO YALIVYOKUWA, KILE KILICHOTOKEA, NA JINSI MAISHA YAKO YALIVYO SASA*. Ikiwa huna ushuhuda ambao unaweza kumwelezea mtu mwingine, unapaswa kusoma kitabu kibinafsi, uombe sala iliyo kwenye ukurasa wa 14 kwa sauti na uamini kile ambacho umesema moyoni mwako. Kisha unaweza kurudi na kuendelea na mazungumzo yako na yule mtu unayemshuhudia. Tazama makala ya *JINSI YA KUTOA USHUHUDA WAKO: USHAHIDI WA KIKRISTO KUPITIA USHUHUDA BINAFSI* iliyo katika kurasa zilizotangulia.



Kristo Ndani Yako
Wakolosai 1:27

• **Uliza swali chochezi.** Muulize rafiki yako ikiwa kile ulichosema kina maana yoyote kwake. Muulize kama anafikiria ataenda mbinguni atakapokufa. Muulize anafikiria maana ya uzima wa milele ni nini. Mshirikishe katika mazungumzo ya kiroho yanayomlenga Kristo. Mungu atakupa maneno ya kusema, unahitaji tu kuwa tayari na wazi.

• **Mwongoze rafiki yako kumpokea Yesu Kristo.** Ikiwa rafiki yako atasema yuko tayari kumpokea Kristo, ("Nataka kuwa na kile ulicho nacho. Je, ni jinsi gani naweza kuwa Mkristo? Nataka kujua mengi zaidi.") mwongoze katika kumpokea Kristo kwa kurudi kwenye sala ya ukurasa wa 14 katika kitabu cha *JINSI YA KUWA MTOTO WA MUNGU* na uumpe nafasi ya kuomba sala hiyo kwa sauti yeye mwenyewe au akirudia baada yako. Baada ya kuomba pamoja naye, pitia maandishi na picha zilizo kwenye kurasa za15-20 ili kuhakikisha kuwa ameelewa mambo yote kuhusu ujumbe wa msalaba. Ikiwa umefuata maagizo yote kikamilifu, kutakuwa na jina jipya lililoandikwa mbinguni na rafiki yako atakuwa mtoto wa Mungu!

## Kuvuna Mavuno

Ukifuata maagizo haya rahisi, utakuwa mtu anayeleta nafsi za watu kwa Kristo. Hakuna swali au sharti lolote. Mungu alikuumba na utu maalum kabisa na nyanja maalum ya ushawishi kwa lengo la kuwavutia watu fulani ambao tayari unawajua. Unachohitaji kufanya ni kuomba kwa dhati na kuwasiliana nao. **Mungu atafanya kile kilichobakia!** Kuna uwezekano mkubwa kwamba watu ulioandika majina yao katika orodha yako ndio hao hao ambao Mungu pia amewachagua. Wanahitaji mtangazaji wa injili tu na huyo atakuwa wewe! **Mungu atanena kupitia wewe unapozungumza na rafiki yako. Amini tu kwamba zoezi hilo lote lilikuwa limeshapangwa hapo awali na Mungu amekuwa akikusubiri uwasili.** Jitolee kutekeleza huduma hiyo kwani hiyo tu ndio Baba anataka. Sharti la pekee ni kwamba huenda wakati sahihi haujafika kwa mtu huyo kumpokea Kristo. Ikiwa hali ni hiyo, basi hutaweza kuleta nafsi ya mtu huyo kwa Yesu siku hiyo, lakini utakuwa mpandaji wa mbegu. Katika hali yoyote ile, utakuwa umemtii Baba yako wa Mbinguni, na ni hilo tu ndilo analotaka. Ikiwa wewe ni mtoto wa Mungu, si wewe kamwe, bali ni Kristo ndani yako ndiye anayetekeleza kazi hiyo.



Mathayo 4:19-20, Mathayo 10:32, Luka 9:60, Luka 10:2, Luka 19:10, Yohana 15:16, Matendo 1:8, Matendo 9:28, 1 Timotheo 2:3-4

## Vifungu vyote vya Bibilia kwa Utaratibu wa Kialfabeti

Ezekieli 36:26-27 Nami nitawapa ninyi moyo mpya, nami nitatia roho mpya ndani yenu, nami nitatoa moyo wa jiwe uliomo ndani ya mwili wenu, nami nitawapa moyo wa nyama. Nami nitatia roho yangu ndani yenu, na kuwaendesha katika sheria zangu, nanyi mtazishika hukumu zangu, na kuzitenda. Ukurasa wa 8

Luka 1:78-79 Kwa njia ya rehema za Mungu wetu, Ambazo kwa hizo mwangaza utokao juu umetufikia, Kuwaangaza wakaao katika giza na uvuli wa mauti, Na kuiongoza miguu yetu kwenye njia ya amani. Ukurasa wa 10

Luka 10:2 Akawaambia, Mavuno ni mengi, lakini wafanya kazi ni wachache; basi mwombeni Bwana wa mavuno apeleke wafanya kazi katika mavuno yake. Ukurasa wa 40

Luka 19:10 Kwa kuwa Mwana wa Adamu alikuja kutafuta na kuokoa kile kilichopotea. Ukurasa wa 40

Luka 2:40 Yule mtoto akakua, akaongezeka nguvu, amejaa hekima, na neema ya Mungu ilikuwa juu yake. Ukurasa wa 3

Luka 2:41-47 Basi, wazee wake huenda Yerusalemu kila mwaka, wakati wa sikukuu ya Pasaka. Na alipofikisha umri wa miaka kumi na miwili, walipanda kama ilivyokuwa desturi ya sikukuu; na walipokwisha kuzitimiza siku, wakati wa kurudi kwao, yule mtoto Yesu alibaki nyuma huko Yerusalemu, na wazee wake walikuwa hawana habari. Nao wakadhani ya kuwa yumo katika msafara; wakaenda mwendo wa kutwa, wakawa wakimtafuta katika jamaa zao na wenzao; na walipomkosa, wakarudi Yerusalemu, huku wakimtafuta. kawa baada ya siku tatu wakamwona hekaluni, ameketi katikati ya waalimu, akiwasikiliza na kuwauliza maswali. Nao wote waliomsikia walistaajabia fahamu zake na majibu yake. Ukurasa wa 3

Luka 2:52 Naye Yesu akazidi kuendelea katika hekima na kimo, akimpendeza Mungu na wanadamu. Ukurasa wa 3

Luka 24:1-7 Siku ya kwanza ya juma, ilipoanza kupambazuka, walikwenda kaburini, wakiyaleta manukato waliyoweka tayari. Wakalikuta lile jiwe limevingirishwa mbali na kaburi, Wakaingia, wasiuone mwili wa Bwana Yesu. Ikawa walipokuwa wakifadhaika kwa ajili ya neno hilo, tazama, watu wawili walisimama karibu nao, wamevaa nguo za kumetameta; nao walipoingiwa na hofu na kuinama kifudifudi hadi nchini, hao waliwaambia, Kwa nini mnamtafuta aliye hai katika wafu? Hayupo hapa, amefufuka. Kumbukeni alivyosema nanyi alipokuwa bado yuko Galilaya, akisema, Imempasa Mwana wa Adamu kutiwa mikononi mwa wenye dhambi, na kusulubiwa, na kufufuka siku ya tatu. Ukurasa wa 5

Luka 24:50-51 Akawaongoza mpaka Bethania, akainua mikono yake akawabariki. Ikawa katika kuwabariki, alijitenga nao; akachukuliwa juu mbinguni. Ukurasa wa 5

Luka 9:60 Akamwambia Waache wafu wawazike wafu wao; bali wewe nenda ukautangaze ufalme wa Mungu. Ukurasa wa 40

Marko 6:2-3 Na ilipokuwa sabato, alianza kufundisha katika sinagogi; wengi waliposikia wakashangaa, wakisema, Huyu ameyapata wapi haya? Na, Ni hekima gani hii aliyopewa huyu? Na, Ni nini miujiza hii mikubwa inayotendeka kwa mikono yake? Huyu si yule seremala, mwana wa Mariamu, na ndugu yao Yakobo, na Yose, na Yuda, na Simoni? Na dada zake hawapo hapa petu? Wakajikwaa kwake. Ukurasa wa 5

Matendo 1:8 Lakini mtapokea nguvu, akiisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu; nanyi mtakuwa mashahidi wangu katika Yerusalemu, na kote katika Yudea, na Samaria, na hata mwisho wa nchi. Ukurasa wa 40

Matendo 4:12 Wala hakuna wokovu katika mwingine awaye yote, kwa maana hapana jina jingine chini ya mbingu walilopewa wanadamu litupasalo sisi kuokolewa kwalo. Ukurasa wa 8

Matendo 9:28 Naye akawa pamoja nao katika Yerusalemu akiingia na kutoka. Akahubiri kwa jina la Bwana kwa ushujaa. Ukurasa wa 40

Mathayo 1:20b-23 Yusufu, mwana wa Daudi, usihofu kumchukua Mariamu mkeo, maana mimba yake ni kwa uweza wa Roho Mtakatifu. Naye atazaa mwana, nawe utamwita jina lake Yesu, maana, yeye ndiye atakayewaokoa watu wake kutoka dhambi zao. Hayo yote yamekuwa, ili litimie neno lililonenwa na Bwana kwa ujumbe wa nabii akisema, Tazama, bikira atachukua mimba, naye atazaa mwana; Nao watamwita jina lake Imanueli; Yaani, Mungu pamoja nasi. Ukurasa wa 1

Mathayo 10:32 Basi, kila mtu atakayenikiri mbele ya watu, nami nitamkiri mbele za Baba yangu aliye mbinguni. Ukurasa wa 40

Mathayo 26:28-29 Kwa maana hii ndiyo damu yangu ya agano, imwagikayo kwa ajili ya wengi kwa ondoleo la dhambi. 29Lakini nawaambieni, Sitakunywa kabisa tangu sasa uzao huu wa mzabibu, hata siku ile nitakapokunywa mpya pamoja nanyi katika ufalme wa Baba yangu. Ukurasa wa 4

Mathayo 27:57-61 Na ilipokuwa jioni akafika mtu tajiri wa Arimathaya, jina lake Yusufu, naye mwenyewe alikuwa mwanafunzi wa Yesu; mtu huyu alimwendea Pilato akaomba apewe mwili wa Yesu. Ndipo Pilato akaamuru apewe. Yusufu akautwaa mwili, akauzongazonga katika sanda ya kitani safi, akauweka katika kaburi lake jipya, alilokuwa amelichonga mwambani; akavingirisha jiwe kubwa mbele ya mlango wa kaburi, akaenda zake. Na pale walikuwapo Mariamu Magdalene, na Mariamu yule wa pili, wameketi kulielekea kaburi. Ukurasa wa 4

Mathayo 3:13-17 Wakati huo Yesu akaja kutoka Galilaya mpaka Yordani kwa Yohana ili abatizwe. Lakini Yohana alitaka kumzuia, akisema, Mimi nahitaji kubatizwa na wewe, nawe waja kwangu? Yesu akajibu akamwambia, Kubali hivi sasa; kwa kuwa ndivyo itupasavyo kuitimiza haki yote. Ndipo akakubali. Naye Yesu alipokwisha kubatizwa mara aliibuka kutoka majini na tazama, mbingu zikamfunukia, akamwona Roho wa Mungu akishuka kama hua, na kutua juu yake; na tazama, sauti kutoka mbinguni ikasema, Huyu ni Mwanangu, mpendwa wangu, ninayependezwa naye. Kurasa za 3 na 26

Mathayo 4:19-20 Akawaambia, Nifuateni, nami nitawafanya kuwa wavuvi wa watu. Mara wakaziacha nyavu zao, wakamfuata. Ukurasa wa 40

Mathayo 7:13-14 Ingieni kwa kupitia mlango ulio mwembamba; maana mlango ni mpana, na njia ni pana iendayo upotevuni, nao ni wengi waingiao kwa mlango huo. Bali mlango ni mwembamba, na njia imebana iendayo uzimani, nao waionao ni wachache. Ukurasa wa 23

Mathayo 7:28-29 Ikawa, Yesu alipoyamaliza maneno hayo, makutano walishangaa mno kwa mafundisho yake; kwa maana alikuwa akiwafundisha kama mtu mwenye mamlaka, wala si kama waandishi wao. Ukurasa wa 3

Mathayo 7:7-8 Ombeni, nanyi mtapewa; tafuteni, nanyi mtaona; bisheni, nanyi mtafunguliwa; kwa maana kila aombaye hupokea; naye atafutaye huona; naye abishaye atafunguliwa. Ukurasa wa 26

Mhubiri 3:11 Kila kitu amekifanya kizuri kwa wakati wake; tena ameiweka hiyo milele ndani ya mioyo yao; ila kwa jinsi mwanadamu asivyoweza kuivumbua kazi ya Mungu anayoifanya, tangu mwanzo hata mwisho. Ukurasa wa 10

Mithali 14:12 Iko njia ionekanayo kuwa sawa machoni pa mtu, Lakini mwisho wake ni njia za mauti. Ukurasa wa 11

Mwanzo 2:16-17 BWANA Mungu akamwagiza huyo mtu, akisema, "Matunda ya kila mti wa bustani waweza kula, Lakini matunda ya mti wa ujuzi wa mema na mabaya usile, kwa maana siku utakapokula matunda ya mti huo utakufa hakika." Ukurasa wa 6

Mwanzo 2:7 BWANA Mungu akamfanya mtu kwa mavumbi ya ardhi, akampulizia puani pumzi ya uhai; mtu akawa kiumbe hai. Ukurasa wa 24

Mwanzo 2:8-9 BWANA Mungu akapanda bustani upande wa mashariki wa Edeni, akamweka ndani yake huyo mtu aliyemfanya. BWANA Mungu akachipusha katika ardhi kila mti unaotamanika kwa macho na kufaa kwa kuliwa; na mti wa uzima katikati ya bustani, na mti wa ujuzi wa mema na mabaya. Ukurasa wa 6

Mwanzo 3:23 Kwa hiyo BWANA Mungu akamtoa katika bustani ya Edeni, ailime ardhi ambayo katika hiyo alitwaliwa. Ukurasa wa 6

Mwanzo 3:2-6 Mwanamke akamwambia nyoka, Matunda ya miti ya bustanini twaweza kula; lakini matunda ya mti ulio katikati ya bustani Mungu amesema, Msiyale wala msiyaguse, msije mkafa. Nyoka akamwambia mwanamke, Hakika hamtakufa, kwa maana Mungu anajua ya kwamba siku mtakayokula matunda ya mti huo, mtafumbuliwa macho, nanyi mtakuwa kama Mungu, mkijua mema na mabaya. Mwanamke alipoona ya kuwa ule mti wafaa kwa chakula, wapendeza macho, nao ni mti wa kutamanika kwa maarifa, basi alichuma matunda yake akala, akampa na mumewe, naye akala. Ukurasa wa 6

1 Petro 1:18-19 Nanyi mfahamu kwamba mlikombolewa si kwa vitu viharibikavyo, kwa fedha au dhahabu; mpate kutoka katika mwenendo wenu usiofaa mlioupokea kwa baba zenu; bali kwa damu ya thamani, kama ya mwana-kondoo asiye na dosari wala waa, yaani, ya Kristo.Ukurasa wa 25

1 Petro 2:24 Yeye mwenyewe alizichukua dhambi zetu katika mwili wake juu ya mti, tukiwa wafu kwa mambo ya dhambi, tuwe hai kwa mambo ya haki; na kwa kupigwa kwake mliponywa. Ukurasa wa 4

1 Petro 3:15 Muwe tayari siku zote kumjibu kila mtu awaulizaye habari za tumaini lililo ndani yenu; lakini kwa upole na kwa heshima. Ukurasa wa 36

1 Petro 3:18Kwa maana Kristo naye aliteswa mara moja kwa ajili ya dhambi, mwenye haki kwa ajili yao wasio haki, ili atulete kwa Mungu; akauawa kimwili, lakini akahuishwa kiroho. Ukurasa wa 12

1 Timotheo 2:3-4 Hili ni zuri, nalo lakubalika mbele za Mungu Mwokozi wetu; ambaye hutaka watu wote waokolewe, na kupata kujua yaliyo kweli. Ukurasa wa 40

1 Timotheo 2:5-6 Kwa sababu Mungu ni mmoja, na mpatanishi kati ya Mungu na wanadamu ni mmoja, Mwanadamu Kristo Yesu; ambaye alijitoa mwenyewe kuwa ukombozi kwa ajili ya wote, utakaoshuhudiwa kwa majira yake. Kurasa za 8 na 12

2 Timotheo 1:7 Maana Mungu hakutupa roho ya woga, bali ya nguvu na ya upendo na ya moyo wa kiasi. Ukurasa wa 21

Ufunuo 12:11 Nao wakamshinda kwa damu ya Mwana-kondoo, na kwa neno la ushuhuda wao; ambao hawakupenda maisha yao hata kufa. Ukurasa wa 36

Ufunuo 19:10 Nami nikaanguka mbele ya miguu yake, ili nimsujudie; akaniambia, Angalia, usifanye hivi; mimi ni mtumishi mwenzako na wa ndugu zako walio na ushuhuda wa Yesu. Msujudie Mungu. Kwa maana ushuhuda wa Yesu ndio roho ya unabii. Ukurasa wa 36

Ufunuo 21:2 Nami nikauona mji ule mtakatifu, Yerusalemu mpya, ukishuka kutoka mbinguni kwa Mungu, umewekwa tayari, kama bibi arusi aliyekwisha kupambwa kwa mumewe.Ukurasa wa 20

Ufunuo 3:20 Tazama, nasimama mlangoni, nabisha; mtu akiisikia sauti yangu, na kuufungua mlango, nitaingia kwake, nami nitakula pamoja naye, na yeye pamoja nami. Ukurasa wa 9

1 Wakorintho 15:22 Kwa kuwa kama katika Adamu wote wanakufa, kadhalika na katika Kristo wote watahuishwa. Kurasa za 17 na 23

1 Wakorintho 15:45-46 Ndivyo ilivyoandikwa, Mtu wa kwanza, Adamu, akawa kiumbe aliye hai; Adamu wa mwisho ni roho yenye kuhuisha. Lakini hautangulii ule wa roho, bali ule wa asili; baadaye huja ule wa roho. Ukurasa wa 6

1 Wakorintho 15:57 Lakini Mungu na ashukuriwe atupaye kushinda kwa Bwana wetu Yesu Kristo. Ukurasa wa 8

1 Wakorintho 2:16 Maana, Ni nani aliyeifahamu nia ya Bwana, amwelimishe? Lakini sisi tunayo nia ya Kristo. Ukurasa wa 22

1 Wakorintho 3:16-18 Hamjui ya kuwa ninyi mmekuwa hekalu la Mungu, na ya kuwa Roho wa Mungu anakaa ndani yenu? Kama mtu akiliharibu hekalu la Mungu, Mungu atamharibu mtu huyo. Kwa maana hekalu la Mungu ni takatifu, ambalo ndilo ninyi. Mtu asijidanganye mwenyewe; kama mtu akijiona kuwa mwenye hekima miongoni mwenu katika dunia hii, na awe mpumbavu, ili apate kuwa mwenye hekima. Kurasa za 24 na 25

1 Wakorintho 6:17 Lakini yeye aliyeungwa na Bwana ni roho moja naye. Kurasa za 15, 16 na 24

1 Wakorintho 6:19-20 Au hamjui ya kuwa mwili wenu ni hekalu la Roho Mtakatifu aliye ndani yenu, mliyepewa na Mungu? Wala ninyi si mali yenu wenyewe; maana mlinunuliwa kwa thamani. Sasa basi, mtukuzeni Mungu katika miili yenu. Ukurasa wa 25

2 Wakorintho 5:16-21 Hata imekuwa, sisi tangu sasa hatumjui mtu awaye yote kwa jinsi ya mwili. Ingawa sisi tumemtambua Kristo kwa jinsi ya mwili, lakini sasa hatumtambui hivi tena. Hata imekuwa, mtu akiwa ndani ya Kristo amekuwa kiumbe kipya; ya kale yamepita, tazama! Yamekuwa mapya. Lakini vyote pia vyatokana na Mungu, aliyetupatanisha sisi na nafsi yake kwa Kristo, naye alitupa huduma ya upatanisho; yaani, Mungu alikuwa ndani ya Kristo, akiupatanisha ulimwengu na nafsi yake, asiwahesabie makosa yao; naye ametia ndani yetu neno la upatanisho. Basi tu wajumbe kwa ajili ya Kristo, kana kwamba Mungu anasihi kwa vinywa vyetu; twawaomba ninyi kwa ajili ya Kristo

mpatanishwe na Mungu. Yeye asiyejua dhambi alimfanya kuwa dhambi kwa ajili yetu, ili sisi tupate kuwa haki ya Mungu katika Yeye. Ukurasa wa 25

2 Wakorintho 5:17 Hata imekuwa, mtu akiwa ndani ya Kristo amekuwa kiumbe kipya; ya kale yamepita, tazama! Yamekuwa mapya.Ukurasa wa 20

2 Wakorintho 5:18 Lakini vyote pia vyatokana na Mungu, aliyetupatanisha sisi na nafsi yake kwa Kristo, naye alitupa huduma ya upatanisho. Ukurasa wa 8

1 Wathesalonike 1:6-8 Nanyi mkawa wafuasi wetu na wa Bwana, mkiisha kulipokea neno katika dhiki nyingi, pamoja na furaha ya Roho Mtakatifu.Hata mkawa kielelezo kwa watu wote waaminio katika Makedonia, na katika Akaya. Maana kutoka kwenu neno la Mungu limevuma, si katika Makedonia na Akaya tu, ila na kila mahali imani yenu mliyo nayo kwa Mungu imeenea; hata hatuna haja sisi kunena lolote. Ukurasa wa 36

1 Wathesalonike 5:23-24 Mungu wa amani mwenyewe awatakase kabisa; nanyi nafsi zenu na roho zenu na miili yenu mhifadhiwe muwe kamili, bila lawama, wakati wa kuja kwake Bwana wetu Yesu Kristo. Yeye ni mwaminifu ambaye awaita, naye atafanya. Kurasa za 24 na 25

Waefeso 1:11 na ndani yake sisi nasi tulifanywa urithi, huku tukichaguliwa tangu awali sawasawa na kusudi lake yeye, ambaye hufanya mambo yote kwa shauri la mapenzi yake. Ukurasa wa 18

Waefeso 1:13-14 Nanyi pia katika huyo mmekwisha kulisikia neno la kweli, Habari Njema za wokovu wenu; tena mmekwisha kumwamini yeye, na kutiwa mhuri na Roho yule wa ahadi aliye Mtakatifu. Ndiye aliye arabuni ya urithi wetu, ili kuleta ukombozi wa milki yake, kuwa sifa ya utukufu wake. Kurasa za 17 na 19

Waefeso 1:5-8 Kwa kuwa alitangulia kutuchagua, ili tufanywe wanawe kwa njia ya Yesu Kristo, kulingana na radhi ya mapenzi yake. Na usifiwe utukufu wa neema yake, ambayo ametuneemesha katika huyo Mpendwa. Katika yeye huyo, kwa damu yake, tunao ukombozi wetu, msamaha wa dhambi, sawasawa na wingi wa neema yake. Naye alituzidishia hiyo katika hekima yote na ujuzi. Kurasa za 15 na 16

Waefeso 1:7 Katika yeye huyo, kwa damu yake, tunao ukombozi wetu, msamaha wa dhambi, sawasawa na wingi wa neema yake. Ukurasa wa 4

Waefeso 2:13 Lakini sasa, katika Kristo Yesu, ninyi mliokuwa mbali hapo kwanza mmekuwa karibu kwa damu yake Kristo.Ukurasa wa 13

Waefeso 2:14 Kwa maana yeye ndiye amani yetu, aliyetufanya sisi sote tuliokuwa wawili kuwa mmoja; akakibomoa kiambaza cha kati kilichotutenga. Ukurasa wa 9

Waefeso 2:6 Akatufufua pamoja naye, akatuketisha pamoja naye katika ulimwengu wa roho, katika Kristo Yesu. Ukurasa wa 19

Waefeso 2:8-10 Kwa maana mmeokolewa kwa neema, kwa njia ya imani; ambayo hiyo haikutokana na nafsi zenu, ni kipawa cha Mungu; wala si kwa matendo, mtu awaye yote asije akajisifu. Kurasa za 8, 15 na 16.

Waefeso 3:14-15 Kwa hiyo nampigia Baba magoti, ambaye kwa jina lake ubaba wote wa mbinguni na wa duniani unaitwa. Ukurasa wa 17

Waefeso 4:21-22 ikiwa kwa hakika mlisikia habari zake na kufundishwa katika yeye, kama kweli ilivyo katika Yesu, mvue mwenendo wenu wa kwanza, utu wa zamani unaoharibika, kwa kuzifuata tamaa zenye kudanganya. Ukurasa wa 25

Wafilipi 2:5-8 Iweni na nia iyo hiyo ndani yenu ambayo ilikuwamo pia ndani ya Kristo Yesu; ambaye yeye mwanzo alikuwa yuko na namna ya Mungu, naye hakuona kule kuwa sawa na Mungu kuwa ni kitu cha kushikamana nacho; bali alijifanya kuwa hana utukufu, akatwaa namna ya mtumwa, akawa ana mfano wa wanadamu; tena, alipoonekana ana umbo kama mwanadamu, alijinyenyekeza akawa mtii hata mauti, naam, mauti ya msalaba. Ukurasa wa 1, 2, 22 na 25

Wafilipi 3:20 Kwa maana sisi, wenyeji wetu uko mbinguni; kutoka huko tena tunamtazamia Mwokozi, Bwana Yesu Kristo. Kurasa za 20, 22 na 23

Wafilipi 4:6-7 Msijisumbue kwa neno lolote; bali katika kila neno kwa kusali na kuomba, pamoja na kushukuru, haja zenu na zijulikane na Mungu. Na amani ya Mungu, ipitayo akili zote, itawahifadhi mioyo yenu na nia zenu katika Kristo Yesu. Ukurasa wa 26

Wagalatia 1:15-16 Lakini Mungu, aliyenitenga tangu tumboni mwa mama yangu, akaniita kwa neema yake, alipoona vema kumdhihirisha Mwanawe ndani yangu, ili niwahubirie Mataifa habari zake; mara sikufanya shauri na watu wenye mwili na damu. Ukurasa wa 8

Wagalatia 2:20 Nimesulubiwa pamoja na Kristo; lakini ni hai; wala si mimi tena, bali Kristo yu hai ndani yangu; na uhai nilio nao sasa katika mwili, ninao katika imani ya Mwana wa Mungu, ambaye alinipenda, akajitoa nafsi yake kwa ajili yangu. Ukurasa wa 18

Wagalatia 4:4-7 Lakini ulipowadia utimilifu wa wakati, Mungu alimtuma Mwanawe ambaye amezaliwa na mwanamke, amezaliwa chini ya sheria, kusudi awakomboe hao waliokuwa chini ya sheria, ili sisi tupate kupokea hali ya kuwa wana. Na kwa kuwa ninyi mmekuwa wana, Mungu alimtuma Roho wa Mwanawe mioyoni mwetu, aliaye, Aba, yaani, Baba. Kama ni hivyo, wewe si mtumwa tena bali u mwana; na kama u mwana, basi, u mrithi kwa Mungu.Ukurasa wa 18

Wagalatia 5:16 Basi nasema, Nendeni kwa Roho, wala hamtazitimiza kamwe tamaa za mwili. Ukurasa wa 23

Wagalatia 5:24 Na hao walio wa Kristo Yesu wameusulubisha mwili pamoja na mawazo yake mabaya na tamaa zake. Kurasa za 17 na 18

Wakolosai 1:15 Naye ni mfano wa Mungu asiyeonekana, mzaliwa wa kwanza wa viumbe vyote. Ukrasa wa 1 na wa 2

Wakolosai 1:26-27 Mungu alipenda kuwajulisha jinsi ulivyo utajiri wa utukufu wa siri hii katika Mataifa, nao ni Kristo ndani yenu, tumaini la utukufu. Ukurasa wa 25

Wakolosai 2:10 Na ninyi mmetimilika katika yeye aliye kichwa cha enzi yote na mamlaka. Ukurasa wa 18

Wakolosai 2:12-14 Mkazikwa pamoja naye katika ubatizo; na katika huo mkafufuliwa pamoja naye, kwa kuziamini nguvu za Mungu aliyemfufua katika wafu.Na ninyi mlipokuwa mmekufa kwa sababu ya makosa yenu na kutotahiriwa kwa mwili wenu, aliwafanya hai pamoja naye, akiisha kutusamehe makosa yote; kiisha kuifuta ile hati iliyoandikwa ya kutushitaki kwa hukumu zake, iliyokuwa na uadui kwetu; akaiondoa isiwepo tena, akaigongomea msalabani. Ukurasa wa 19

Wakolosai 2:6-7 Basi kama mlivyompokea Kristo Yesu, Bwana, ishini vivyo hivyo katika yeye; wenye shina na wenye kujengwa katika yeye; mmefanywa imara kwa imani, kama mlivyofundishwa; mkizidi kutoa shukrani. Kurasa za 15 na16

Wakolosai 2:9 Maana katika yeye unakaa utimilifu wote wa Mungu, kwa jinsi ya kimwili. Ukurasa wa 1 na wa 2

Wakolosai 3:1-3 Basi mkiwa mmefufuliwa pamoja na Kristo, yatafuteni yaliyo juu Kristo aliko, ameketi katika mkono wa kulia wa Mungu. Yafikirini yaliyo juu, siyo yaliyo katika nchi. Kwa maana mlikufa, na uhai wenu umefichwa pamoja na Kristo katika Mungu.Ukurasa wa 19

Wakolosai 4:5-6 Nendeni kwa hekima mbele yao walio nje, mkiukomboa wakati. Maneno yenu yawe na neema siku zote, yakikolezwa chumvi, ili mpate kujua jinsi iwapasavyo kumjibu kila mtu. Ukurasa wa 36

Waraka kwa Waebrania 1:3 Yeye kwa kuwa ni mng>ao wa utukufu wa Mungu na chapa kamili ya nafsi yake, akivichukua vyote kwa amri ya uweza wake, akiisha kufanya utakaso wa dhambi, aliketi katika mkono wa kulia wa Ukuu huko juu. Ukurasa wa 1, 2 na 5

Waraka kwa Waebrania 2:11-17 Maana yeye atakasaye na hao wanaotakaswa wote pia watoka kwa mmoja. Kwa ajili hii haoni haya kuwaita ndugu zake; akisema, Nitalihubiri jina lako kwa ndugu zangu; Katikati ya kanisa nitakuimbia sifa. Na tena, Nitakuwa nimemtumaini yeye. Na tena, Tazama, mimi nipo hapa na watoto niliopewa na Mungu. Basi, kwa kuwa watoto wameshiriki damu na mwili, yeye naye vivyo hivyo alishiriki yayo hayo, ili kwa njia ya mauti amharibu yeye aliyekuwa na nguvu za mauti, yaani, Ibilisi, 15awaache huru wale ambao katika maisha yao yote kwa hofu ya mauti walikuwa katika hali ya utumwa. Maana ni hakika, hatwai asili ya malaika, ila atwaa asili ya mzao wa Abrahamu. Hivyo ilimpasa kufananishwa na ndugu zake katika mambo yote, apate kuwa kuhani mkuu mwenye rehema, mwaminifu katika mambo ya Mungu, ili afanye kafara ya suluhu kwa dhambi za watu wake. Ukurasa wa 1, 2 na 20

Waraka kwa Waebrania 2:14-15 Basi, kwa kuwa watoto wameshiriki damu na mwili, yeye naye vivyo hivyo alishiriki yayo hayo, ili kwa njia ya mauti amharibu yeye aliyekuwa na nguvu za mauti, yaani,

Ibilisi, awaache huru wale ambao katika maisha yao yote kwa hofu ya mauti walikuwa katika hali ya utumwa. Ukurasa wa 4

Waraka kwa Waebrania 4:12 Maana neno la Mungu li hai, tena lina nguvu, tena lina ukali kuliko upanga uwao wote ukatao kuwili, tena lachoma hata kuzigawanya nafsi na roho, na viungo na mafuta yaliyomo ndani yake; tena ni jepesi kuyatambua mawazo na makusudi ya moyo. Kurasa za 24 na 26

Waraka kwa Waebrania 4:3 Maana sisi tulioamini tunaingia katika pumziko lile; kama vile alivyosema, Kama nilivyoapa kwa hasira yangu, Hawataingia pumzikoni mwangu: ijapokuwa zile kazi zilimalizika tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu.Ukurasa wa 13

Waraka kwa Waebrania 4:7 Mungu aweka tena siku fulani, akisema katika Daudi baada ya muda mwingi namna hii, Leo, kama ilivyonenwa tangu zamani, Leo, kama mkisikia sauti yake, Msifanye mioyo yenu migumu. Ukurasa wa 13

Waraka kwa Waebrania 9:22 Na katika Torati karibu vitu vyote husafishwa kwa damu, na pasipo kumwaga damu hakuna ondoleo. Ukurasa wa 4

Warumi 10:13 kwa kuwa, Kila atakayeliitia Jina la Bwana ataokoka. Kurasa za 15 na 16

Warumi 12:1 Basi, ndugu zangu, nawasihi, kwa huruma zake Mungu, itoeni miili yenu iwe dhabihu iliyo hai, takatifu, ya kumpendeza Mungu, ndiyo ibada yenu yenye maana. Ukurasa wa 25

Warumi 12:4-5 Kwa kuwa kama vile katika mwili mmoja tuna viungo vingi, wala viungo vyote havitendi kazi moja; Vivyo hivyo na sisi tulio wengi tu mwili mmoja katika Kristo, na viungo, kila mmoja kwa mwenzake. Ukurasa wa 25

Warumi 3:23 Kwa sababu wote wamefanya dhambi, na kupungukiwa na utukufu wa Mungu. Kurasa za 7 na 11

Warumi 5:11 Wala si hivyo tu, ila pia twajifurahisha katika Mungu kwa Bwana wetu Yesu Kristo, ambaye kwa yeye sasa tumeupokea huo upatanisho. Ukurasa wa 20

Warumi 5:1-2 Basi tukiisha kuhesabiwa haki itokayo katika imani, na muwe na amani kwa Mungu, kwa njia ya Bwana wetu Yesu Kristo, ambaye kwa yeye tumepata kwa njia ya imani kuifikia neema hii ambayo mnasimama ndani yake; na kufurahi katika tumaini la utukufu wa Mungu. Kurasa za 10 na 12

Warumi 5:12 Kwa hiyo, kama kwa mtu mmoja dhambi iliingia ulimwenguni, na kwa dhambi hiyo mauti; na hivyo mauti ikawafikia watu wote kwa sababu wote wamefanya dhambi. Ukurasa wa 7

Warumi 5:18-19 Basi tena, kama kwa kosa moja watu wote walihukumiwa adhabu, kadhalika kwa tendo moja la haki watu wote walihesabiwa haki yenye uzima. Kwa sababu kama kwa kuasi kwake mtu mmoja watu wengi waliingizwa katika hali ya wenye dhambi, kadhalika kwa kutii kwake mmoja watu wengi wameingizwa katika hali ya wenye haki. Kurasa za 7 na 17

Warumi 5:5 Na tumaini halitahayarishi; kwa maana pendo la Mungu limekwisha kumiminwa katika mioyo yetu na Roho Mtakatifu tuliyepewa sisi. Ukurasa wa 19

Warumi 5:6 Kwa maana hapo tulipokuwa hatuna nguvu, wakati ulipotimia, Kristo alikufa kwa ajili ya waovu. Ukurasa wa 4

Warumi 5:9 Basi zaidi sana tukiisha kuhesabiwa haki katika damu yake, tutaokolewa na ghadhabu kwa yeye.Ukurasa wa 8

Warumi 6:11-13 Vivyo hivyo ninyi nanyi jihesabuni kuwa wafu kwa dhambi na walio hai kwa Mungu katika Kristo Yesu. Basi, dhambi isitawale ndani ya miili yenu ipatikanayo na mauti, hata mkazitii tamaa zake; wala msiendelee kuvitoa viungo vyenu kuwa silaha za dhuluma kwa dhambi; bali jitoeni wenyewe kwa Mungu kama walio hai baada ya kufa, na viungo vyenu kwa Mungu kuwa silaha za haki. Ukurasa wa 25

Warumi 6:16 Hamjui ya kuwa kwake yeye ambaye mnajitoa nafsi zenu kuwa watumwa wake katika kumtii, mmekuwa watumwa wake yule mnayemtii, iwe ni utumishi wa dhambi uletao mauti, au iwe ni utumishi wa utii uletao haki. Kurasa za 9 na 23

Warumi 6:21 Hamjui ya kuwa kwake yeye ambaye mnajitoa nafsi zenu kuwa watumwa wake katika kumtii, mmekuwa watumwa wake yule mnayemtii, iwe ni utumishi wa dhambi uletao mauti, au iwe ni utumishi wa utii uletao haki. Ukurasa wa 9

Warumi 6:23 Kwa maana mshahara wa dhambi ni mauti; bali karama ya Mungu ni uzima wa milele katika Kristo Yesu Bwana wetu. Ukurasa wa 11

Warumi 6:4-6 Basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake, kusudi kama Kristo alivyofufuka katika wafu kwa njia ya utukufu wa Baba, vivyo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima. Kwa maana kama mlivyounganika naye katika mfano wa mauti yake, kadhalika mtaunganika kwa mfano wa kufufuka kwake; mkijua neno hili, ya kuwa utu wetu wa kale ulisulubishwa pamoja naye, ili mwili wa dhambi ubatilike, tusitumikie dhambi tena. Kurasa za 18 na 19

Warumi 7:14-25 Kwa maana twajua ya kuwa torati asili yake ni ya rohoni; bali mimi ni mtu wa mwilini, nimeuzwa chini ya dhambi. Maana sijui nifanyalo, kwa sababu lile nilipendalo, silitendi; bali lile nilichukialo ndilo ninalolitenda. Lakini kama nikilitenda lile nisilolipenda, naikiri ile sheria ya kuwa ni njema. Basi sasa si mimi nafsi yangu ninayetenda hilo, bali ni ile dhambi ikaayo ndani yangu Kwa maana najua ya kuwa ndani yangu, yaani, ndani ya mwili wangu, halikai neno jema; kwa kuwa kutaka nataka, bali kutenda lililo jema siwezi. Kwa maana lile jema nilipendalo, silitendi; bali lile baya nisilolipenda ndilo nilitendalo. Basi kama lile nisilolipenda ndilo nilitendalo, si mimi nafsi yangu nilitendaye, bali ni ile dhambi ikaayo ndani yangu. Basi nimeona sheria hii, ya kuwa kwangu mimi nitakaye kutenda lililo jema, lipo lililo baya. Kwa maana naifurahia sheria ya Mungu kwa utu wa ndani, lakini katika viungo vyangu naona sheria iliyo mbali, inapiga vita na ile sheria ya akili zangu, na kunifanya mateka wa ile sheria ya dhambi iliyo katika viungo vyangu. Ole wangu, maskini mimi! Ni nani atakayeniokoa na mwili huu wa mauti? Namshukuru Mungu, kwa Yesu Kristo Bwana wetu. Basi, kama ni hivyo, mimi mwenyewe kwa akili zangu naitumikia sheria ya Mungu, bali kwa mwili wangu sheria ya dhambi. Ukurasa wa 23

Warumi 8:10 Na Kristo akiwa ndani yenu, mwili wenu umekufa kwa sababu ya dhambi; bali roho yenu i hai, kwa sababu ya haki.Kurasa za 19, 4 na 25

Warumi 8:1-2 Sasa, basi, hakuna hukumu ya adhabu juu yao walio katika Kristo Yesu. Kwa sababu sheria ya Roho wa uzima ule ulio katika Kristo Yesu imeniacha huru, mbali na sheria ya dhambi na mauti. Kurasa za 17 na 23

Warumi 8:15-17a Kwa kuwa hamkupokea tena roho wa utumwa iletayo hofu; bali mlipokea roho ya kufanywa wana, ambayo kwa hiyo twalia, Aba, yaani, Baba. Roho mwenyewe hushuhudia pamoja na roho zetu, ya kuwa sisi tu watoto wa Mungu; na kama tu watoto, basi, tu warithi; warithi wa Mungu, warithio pamoja na Kristo. Kurasa za 20 na 21

Warumi 8:3 Maana yale yasiyowezekana kwa sheria, kwa vile ilivyokuwa dhaifu kwa sababu ya mwili, Mungu, kwa kumtuma Mwanawe mwenyewe katika mfano wa mwili ulio wa dhambi, na kwa sababu ya dhambi, aliihukumu dhambi katika mwili. Ukurasa wa 1, 2, na 4

Warumi 8:37 Lakini katika mambo hayo yote sisi ni zaidi ya washindi, kupitia kwake yeye aliyetupenda. Ukurasa wa 9

Warumi 8:5-6 Kwa maana wale waufuatao mwili huyafikiri mambo ya mwili; bali wale waifuatao roho huyafikiri mambo ya roho. Kwa kuwa nia ya mwili ni mauti; bali nia ya roho ni uzima na amani. Kurasa za 17 na 23

Warumi10:9 Kwa sababu, ukimkiri Yesu kwa kinywa chako ya kuwa ni Bwana, na kuamini moyoni mwako ya kuwa Mungu alimfufua katika wafu, utaokoka. Kurasa za 15 na 16

Yakobo 5:16 Basi ungameni dhambi zenu ninyi kwa ninyi, na kuombeana, ili mpate kuponywa. Sala yake mwenye haki ina nguvu nyingi, na hutenda mengi. Ukurasa wa 26

1 Yohana 1:7 Bali tukienenda katika nuru, kama yeye alivyo katika nuru, tunashirikiana sisi kwa sisi, na damu yake Yesu, Mwana wake, yatusafisha dhambi yote. Ukurasa wa 4

1 Yohana 1:9 Tukiziungama dhambi zetu, Yeye ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee dhambi zetu, na kututakasa na udhalimu wote. Ukurasa wa 26

1 Yohana 3:1-3 Tazameni, ni pendo la namna gani alilotupa Baba, kwamba tuitwe wana wa Mungu; na ndivyo tulivyo. Kwa sababu hii ulimwengu haututambui, kwa kuwa haukumtambua yeye. Wapenzi, sasa tu wana wa Mungu, wala haijadhihirika bado tutakavyokuwa; lakini tunajua ya kuwa atakapodhihirishwa, tutafanana naye; kwa maana tutamwona kama alivyo. Na kila mwenye matumaini haya katika yeye hujitakasa, kama yeye alivyo mtakatifu. Ukurasa wa 25

1 Yohana 3:9-10 Kila mtu aliyezaliwa na Mungu hatendi dhambi, kwa sababu uzao wake wakaa ndani yake; wala hawezi kutenda dhambi kwa sababu amezaliwa kutokana na Mungu. Katika hili watoto wa Mungu ni dhahiri, na watoto wa Ibilisi nao. Mtu yeyote asiyetenda haki hatokani na Mungu, wala yeye asiyempenda ndugu yake. Ukurasa wa 25

1 Yohana 5:12-13 2 Yeye aliye naye Mwana, anao huo uzima; asiye naye Mwana wa Mungu hana huo uzima. Nimewaandikia ninyi mambo hayo, ili mjue ya kuwa mna uzima wa milele, ninyi mnaoliamini Jina la Mwana wa Mungu. Kurasa za 15 na 16

1 Yohana 5:18-19 Tunajua ya kuwa kila mtu aliyezaliwa na Mungu hatendi dhambi; bali yeye aliyezaliwa na Mungu hujilinda, wala yule mwovu hamgusi. Tunajua ya kuwa sisi tu wa Mungu; na dunia yote pia hukaa katika yule mwovu. Ukurasa wa 17

Yohana 1:14 Naye Neno alifanyika mwili, akakaa kwetu; nasi tukauona utukufu wake, utukufu kama wa Mwana pekee atokaye kwa Baba; amejaa neema na kweli. Ukurasa wa 1 na wa 2

Yohana 10:10 Mwizi huja tu kuiba, kuua na kuharibu; mimi nilikuja ili wawe na uzima, tena wawe nao tele. Ukurasa wa 9

Yohana 10:30 Mimi na Baba tu mmoja. Ukurasa wa 1 na wa 2

Yohana 11:25-26 Yesu akamwambia, Mimi ndimi huo ufufuo, na uzima. Yeye aniaminiye mimi, hata akifa, atakuwa anaishi; naye kila aishiye na kuniamini hatakufa kabisa hata milele. Je! Unayasadiki hayo? Kurasa za 15, 16, na 19

Yohana 12:17 Basi wakamshuhudia wale mkutano waliokuwapo pamoja naye alipomwita Lazaro kutoka kaburini, akamfufua.Ukurasa wa 36

Yohana 14:13-14 Nanyi mkiomba lolote kwa jina langu, hilo nitalifanya, ili Baba atukuzwe ndani ya Mwana. Mkiniomba neno lolote kwa jina langu, nitalifanya.Ukurasa wa 26

Yohana 14:20 Siku ile ninyi mtatambua ya kuwa mimi ni ndani ya Baba yangu, nanyi ndani yangu, nami ndani yenu. Kurasa za 18 na 19

Yohana 14:6-7 Yesu akamwambia, Mimi ndimi njia, na kweli, na uzima; mtu haji kwa Baba, ila kwa njia ya mimi Kama mngalinijua mimi, mngalimjua na Baba; tangu sasa mnamjua, tena mmemwona. Kurasa za 13, 15 na 16

Yohana 15:16 Si ninyi mlionichagua mimi, bali ni mimi niliyewachagua ninyi; nami nikawaweka mwende mkazae matunda; na matunda yenu yapate kukaa; ili kwamba lolote mmwombalo Baba kwa jina langu awapeni. Ukurasa wa 40

Yohana 15:7 Ninyi mkikaa ndani yangu, na maneno yangu yakikaa ndani yenu, ombeni lolote mtakalo nanyi mtatendewa. Ukurasa wa 26

Yohana 16:28 Nilitoka kwa Baba, nami nimekuja hapa ulimwenguni; tena nauacha ulimwengu; na kwenda kwa Baba.Ukurasa wa 5

Yohana 16:33 Hayo nimewaambieni mpate kuwa na amani ndani yangu. Ulimwenguni mnayo dhiki; lakini jipeni moyo; mimi nimeushinda ulimwengu.Ukurasa wa 10

Yohana 3:16 Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele. Ukurasa wa 12

Yohana 3:6 Kilichozaliwa kwa mwili ni mwili; na kilichozaliwa kwa Roho ni roho. Kurasa za 19 na 24

Yohana 9:25 Basi yule mtu akajibu, Kwamba yeye ni mwenye dhambi sijui. Najua neno moja, kuwa mimi nilikuwa kipofu na sasa naona. Ukurasa wa 36

Yoshua 1:8 Kitabu hiki cha torati kisiondoke kinywani mwako, bali yatafakari maneno yake mchana na usiku, upate kuangalia kutenda kulingana na maneno yote yaliyoandikwa humo; maana ndipo utakapoifanikisha njia yako, kisha ndipo utakapositawi sana. Ukurasa wa 26

Zaburi 16:11 Utanijulisha njia ya uzima; Mbele za uso wako kuna furaha tele; Na katika mkono wako wa kuliaMna mema ya milele. Ukurasa wa 20

Zaburi 40:3 Akatia wimbo mpya kinywani mwangu, Ndio sifa zake Mungu wetu. Wengi wataona na kuogopa, Nao watamtumainia BWANA. Ukurasa wa 36

## Rasilimali za ziada ambazo zinaweza kununuliwa kupitia Amazon au maduka ya vitabu vya Kikristo.


- Injili iliyobaki, Dan Stone na David Gregory
- Ukristo wa Msingi, Bob George
- Mwongozo wa Kupata Furaha, Charles Solomon
- Masuala Kuhusu Kukataliwa, Charles Solomon
- Dhamana ya Maisha Yote, Bill Gillham
- Maisha ya Kawaida ya Kikristo, Bill Gillham
- Keti Tembea Simama, Watchman Nee
- Kuachiliwa kwa Roho, Watchman Nee
- Haki ya Kuzaliwa, David Needham
- Mzabibu wa Kweli, Andrew Murray
- Kukaa Ndani ya Kristo, Andrew Murray
- Kujisalimisha Kikamilifu, Andrew Murray
- Ushindi Katika Kristo, Charles Trumbull
- Ufunguo wa Kuishi kwa Ushindi, Jack Taylor
- Maisha ya Kristo Yaokoayo, W. Ian Thomas
- Karama ya Msamaha, Charles Stanley
- Baraka ya Kuvunjika, Charles Stanley
- Dhiki, Charles Stanley
- Kujidhihirisha Jinsi Ulivyo, John Lynch
- Kujitoa Kwangu Kikamilifu kwa Yule Aliye Juu Sana (kitabu cha ibada za kibinafsi), Oswald Chambers
- Umesamehewa Milele, Bob George
- Uamsho wa Neema, Charles Swindoll
- Kristo Anatosha, John MacArther
- Siri ya Kiroho ya Hudson Taylor, Dkt. Howard Taylor na Bi Howard Taylor
- Ibada za kibinafsi za GraceNotes za kila wiki katika mfumo wa kielektroniki (mtandaoni), John Woodward. Zinapatikana kupitia www.GraceNotebook.com
- Kwangu Kuishi ni Kristo, Kozi ya mafunzo ya kikundi, Charles Solomon
- Msalaba, Ushindi Wako Leo, Mfululizo wa CD uliotayarishwa na Dkt. Charles Stanley (pamoja na mahubiri mengi ya Dkt. Charles Stanley)
- Uzuiaji wa Neema, Lee LeFebre
- Kongamano la Utambulisho Mpya, Mfululizo wa CD uliotayarishwa na Lee LeFebre
- Huru Hatimaye, Tony Evans
- Dkt. Tony Evans (mahubiri yake mengi)
- Gregory Dickow (mahubiri yake mengi)
- Warumi: Sura ya 5-8, Toleo lolote la Biblia
- www.gracefellowshipintl.com
- www.thelifebookstore.com
- Kumtafuta Mungu kupitia Maombi na Kutafakari, David Howell

Uko Hai Kikamilifu na Huru Hatimaye, David Howell

Place Stamp Here

Prison Evangelism, Inc.
PO Box 571977 Houston,
Texas 77257

72019




Ningependa kujua kwa undani zaidi. Tafadhali nitumie nakala ya bila malipo ya "KUMTAFUTA MUNGU KUPITIA MAOMBI NA KUTAFAKARI."

Jina ______________________________

Anwani ____________________________

Mji, nchi, Msimbo wa Posta ______________

______________________________________

Tafadhali tuambie una maoni gani kuhusu "Jinsi ya Kuwa Mtoto wa Mungu." __________

______________________________________

______________________________________

______________________________________

______________________________________

______________________________________

______________________________________


______________________________________

______________________________________

______________________________________

Prison Evangelism, Inc. PO Box 571977 Houston Texas 77257

# JINSI YA KUWA
# *Mtoto wa Mungu*



Pata uzoefu wa kweli hizi rahisi zilizoelezwa kwa michoro na ujifunze jinsi kumtumainia Mungu na kumwamini kunakuwezesha kuishi maisha yenye kuridhisha, yenye utele na yenye ushindi.

JINSI YA KUTUMIA KITABU HIKI:

- Kama njia na mwongozo wa kupata amani na Mungu
- Kama njia ya kuelewa uzoefu wa wokovu
- Kama mafundisho ya Biblia ya kibinafsi au ya kikundi (kuna vifungu 223 vya Biblia)
- Kama kitabu cha ibada za kibinafsi cha siku 30 na mwongozo wa kutafakari wa siku 30, ukitumia vifungu vya Biblia

Mwandishi David Howell ni mtoto wa Mungu aliyeokoka. Taarifa zilizo katika kitabu hiki zinaonyesha kiini cha uzoefu, nguvu na tumaini alilopewa na Yesu Kristo baada ya miaka mingi ya kuishi maisha ya ubinafsi. Kupitia michoro, vifungu vya Biblia na maandishi; Howell anaonyesha jinsi kumwamini na kumuelewa Yesu Kristo na uzoefu wa wokovu ni hali zinazomwezesha mtu kuishi maisha yenye ushindi, utele na amani na Mungu hapa duniani.

Nimesulubiwa pamoja na Kristo; lakini ni hai; wala si mimi tena, bali Kristo yu hai ndani yangu; na uhai nilio nao sasa katika mwili, ninao katika imani ya Mwana wa Mungu, ambaye alinipenda, akajitoa nafsi yake kwa ajili yangu.
Wagalatia 2:20

ISBN 978-0-578-14157-2
90000>
9 780578 141572